



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THIRD ASSEMBLY-THIRD SESSION

THE HANSARD

Tuesday, 12th March 2024

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9:30 a.m.*

[The Speaker (Hon. Mwambire) in the Chair]

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

VISITING STUDENTS FROM MJANAHERI SECONDARY SCHOOL AND OFFICERS FROM SHINNING HOPE FOR COMMUNITY ORGANIZATION (SHOFCO)

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, I have a Communication to make. I would like to acknowledge the presence in the public gallery this morning of students and teachers from Mjanaheri Secondary School and Officers from Shinning Hope for Community Organization (SHOFCO). The students, teachers, and officers from SHOFCO are here for a study visit to appreciate the legislative procedures, practices, traditions, and parliamentary proceedings.

I request that each student, teacher, and officer stand when called upon so that they may be acknowledged in the parliamentary tradition and practice.

Hon. Members, on behalf of the County Assembly of Kilifi and my behalf, I welcome them to the Assembly and wish them well. Let me go through the names so that at least you can appreciate their presence in the parliamentary way: -

1. Esther Mwaka

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

2. Halima Juma
3. Loice Tatu
4. Lucy Kache
5. Purity Pendo
6. Lavenda Tatu
7. Mary Pendo
8. Purity Mapenzi
9. Loice Nguma
10. Daniella Sabato
11. Alice Kabibi
12. Sharlet Kadzo
13. Marriam Emmanuel
14. Elizabeth Tatu
15. Mactilda John
16. Marriam Ngonyo
17. Glorine Fatuma
18. Janet Rehema
19. Katana Riziki
20. Eunice Dama
21. Monica Kahindi
22. Charo Alice
23. Roseline Kadzo
24. Sofia Wario
25. Rachael Munga
26. Salama Lawrence
27. Macrina Kadzo
28. Purity Pendo
29. Alexandra Kadzo
30. Rehema Mheri
31. Loice Sebe
32. Mercy John
33. Mapenzi Wilson
34. Mapenzi Rachael
35. Constance Rehema
36. Peterson Chadi
37. Kelvin Kheri
38. Jenifa Nuru
39. Loveline Khonde
40. Merciline Rehema
41. Rahilu Mohammed
42. Shamim Kombo
43. Pamela Charo.

Teachers: -

1. Ilikori Joel Aluku
2. Charles Kirimo

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

3. Winnie Odhiambo

Hon. Members, allow me now to call upon hon. Paul Charo who is the Member for Magarini Ward to be the first one to welcome the visitors, especially the students.

Hon. Paul: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Kusema kweli, leo ni siku nzuri ambayo tumepokea wageni ambao wamefika Bunge hili la Gatuzi la Kilifi. Nataka niwakaribishe wanafunzi wa shule ya upili ya Mjanaheri. Hii shule iko karibu sana na makazi yangu pale Mjanaheri, basi ninayo furaha kuwaona wamefika katika Bunge hili ili waweze kuona kile tunachokifanya hapa. Waheshimiwa wenzangu, naomba tuwakaribishe wanafunzi hawa ambao wamekuja kututembelea hapa na vile vile wale wageni wengine. Langu nataka niwapongeze walimu ambao wameweza kuja kuwaleta wanafunzi hawa kuja kusoma. Mmefanya jambo la busara ili wajue ya kwamba Bunge la Kilifi linakaa vipi, na ni vitu gani vinaendelea katika Bunge hili.

Pili, nataka niwaambie wanafunzi, sisi mnaotuaona hapa tulipitia mafunzo shuleni kama vile nyinyi na hatimaye kwa sababu ya elimu imetufanya sisi tumefika hapa tumefika. Nina imani nyinyi mkiendelea na masomo vizuri, kwa bidii, Mungu akiwaajalia, tunataka viongozi ambao watasimama kama sisi tulio hapa Bungeni. Nimekuwa mstari wa mbele kule nyumbani kuwaambia ya kwamba elimu ndio msingi wa maisha.

Nina imani ya kwamba njia ambayo mmeishika hata mnapotoka hapa mzingatie masomo na msikize waalimu vile wanavyowambia pale shuleni. Panapo maajaliwa, ipo siku mmoja wenu atakuwa kiongozi awe hapa katika Bunge hili.

Kwa hayo mengi, mheshimiwa Spika, tunawakaribisha katika Bunge hili na isiwe ni mwisho. Leo tuko na biashara kidogo lakini wakati wa mijadala wawe wanapatikana maana Bunge hili ndio linafanya maamuzi ya Gatuzi hili la Kilifi. Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Mungu awabariki. Tutaonana huko nyanjani.

The Speaker (Hon.Mwambire): For fair acknowledgement, Hon. Members, allow me to include the list of SHOFCO who have management to come to the Assembly so that as we acknowledge, you know who you are doing it to. The list is also here. Kindly acknowledge them in the parliamentary way: -

1. Amani Kombo Oscar
2. Magret Nyale Mbodze
3. Swaleh Tsuma
4. Zulpha Umazi Tsuma
5. William Fondo
6. Andrew Ngala Chome
7. Ruth Kabibi Ruwa
8. Elinah Kadzo Mwangala
9. Edward Chiro Kai
10. Emmanuel Kai Mrima
11. David Fadhili
12. Rajab Mramba Mweni
13. Edward Malanga
14. Innocent Ochieng
15. Hilton Munga Juma
16. Ali Mjera Abdallah

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

17. Edward Shabaki
18. Tarzan Mbitha
19. Ismail Mohammed
20. Winnie Deche
21. Shauri Thaki
22. Karembo Naomi
23. Edwin Mwachunga
24. Daniel Rongoma
25. Zainab Mohammed
26. Emmanuel Muthui
27. Patience Salama
28. Catherine Gathura
29. Calvin Mae
30. Salama Mnyazi
31. Elina Dogo
32. Isaack Bayah
33. Ibrahim Gachihi Mwasindo

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, the list is just like the other one where the gender ‘F’ (female) is more than the gender ‘M’ (male). It is good that people are keen on that. Hon. Leader of Majority, it is good that you also share your acknowledgement for the visitors.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, mheshimiwa Spika. Kabla sijaendelea, kuna mheshimiwa ambaye ameingia saa hii na mavazi yake si ya nidhamu. Tuko na wanafunzi na ni lazima tuonyeshe msimamao mwema, kwa hivyo ni atoke nje akatengeneze mavazi yake.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Moses Kea, I beg you to take leave so that you can be appropriately dressed. Serjeants please, assist him in moving out of the Chamber so that he can come back well-dressed.

(Hon. Kea withdrew from the Chamber)

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, mheshimiwa Spika. Ni mfano bora tumeonyesha kwa wanafunzi ya kwamba Bunge hili lina sheria. Pia, nataka kuwakaribisha SHOFKO kwa kututembelea hapa. Mimi ambaye nimesimama hapa, kwa majina naitwa Ibrahim Abdi Athman. Mimi ni *elected MCA* wa Wadi ya Watamu eneo Bunge la Kilifi *North* na ni Kiongozi wa Wengi katika Bunge hili. Nataka kuwakaribisha hapa, mmetupatia moyo na furaha kwa kuja kwenu na isiwe tu ni kwa leo, tunaomba muwe mkitembelea Bunge hili ili mpate ufahamu zaidi pia muangalie kile ambacho kinatendeka katika Bunge hili.

Ni haki yenu kujua, ni haki yenu kufuatilia na ni haki yenu kufika hapa kujua waheshimiwa wenu wanawajibika vipi kikazi. Lengo kubwa, SHOFKO nafikiri mmetimiza umri wa kupiga kura wengi wenu na kwa vile mko karibu na wananchi mnatafikana pia muangalie utendakazi wa waheshimiwa. Mkihubiri mipangilio yenu pia mhubiri mipangilio ya waheshimiwa; ni nani ambaye hatendi kazi katika Bunge hili. Mtakuwa pia mnatupatia morali na wananchi pia wanapata *information* kutoka kwenu kwa sababu si sote ambao tunachapa kazi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Si Bunge hili tu, hata Bunge la Kitaifa huwa linatoa takwimu kila mwaka; yule *the best* na yule *the worst*. Hapa pia tuko nayo, lakini hatuwezi kuwataja kwa sababu si ruhusa yangu mimi, ni nyinyi sasa kufanya utafiti wenu ili kufikisha ujumbe huo kwa wananchi.

Wanafunzi karibuni, mumemsikia mheshimiwa wenu ameongea hapa ndani ya hili Bunge, nataka kuambia wanafunzi kuna sheria, huko sheria mko na *prefect*, sasa mimi ndio Kiongozi wa Wengi, mimi ndio kama *prefect* wa hawa waheshimiwa. Pia, usione ya kwamba hatupambani na vituko, vile ambavyo mnapambana navyo shule, hapa pia tunapambana navyo. Kwa hivyo lazima pia tunatoa muongozo.

Nataka kuwaambia wanafunzi kitu cha muhimu ni kuweka bidi; hapa ndani yetu tuko na *Engineers*, wameomba kura kwa wananchi wamefika hapa, tuko na *Accountants*, tuko na madaktari pia, tuko na wale ambao walikuwa hawana kazi, wameomba kura kwa wananchi wamefika hapa. Kwa hivyo, Bunge hili limejaa waheshimiwa tofauti tofauti.

Kwa hivyo, langu mimi nataka niwaambie wanafunzi nyinyi huwa mnafanya mtihani na kikubwa kufurahika kwenu ni ule mtihani ambao mnapata *marks* nyingi ndio msonge mbele. Sisi mitihani yenu ni utendakazi kwa yule mwananchi. Nyinyi mnakaa *secondary* miaka minne, sisi tunakaa miaka mitano. Ndio unakuta mnajuana nyinyi kama wanafunzi, mnajuana nani ni mwerevu zaidi na nani mjinga zaidi kulingana na na ile mitihani kadri inavyokuja. Hata sisi pia tunajuana, tunajua ni nani ambaye hatorudi katika hili Bunge lakini hatuwezi kuambiana...

(Laughter)

Kwa hivyo, nataka kuwapatia morali wanafunzi ya kwamba hapa msiogope; hapa ni mahali ya kwamba mnasoma mambo mengi sana. Tunatunga sheria katika jimbo letu, ningefurahi mngekuja kesho kwa sababu tunampokea Gavana kuja kuhutubia Bunge hili kesho ambayo huwa ni sheria kila mwaka; yeye na Seneta wetu katika Bunge hili huwa wanahutubia kila mwaka. Seneta alikuja wiki iliyopita na Gavana anakuja kesho mchana. Ningefurahi mheshimiwa kama utakuwa na uwezo na mimi naamini uko na uwezo uwaletе wanafunzi waje wasikie hotuba ya Gavana wao.

SHOFCO pia kesho mkipata nafasi ni siku nzuri katika Bunge hili; ni siku nzuri tutakuwa na Gavana wetu akihutubia Bunge letu, msikie yale ambayo atakuwa ameyatenda na yale ambayo tunayatarajia kuyatenda katika serikali hii. Kwa hivyo, mimi langu ni kutaka kuwaambia wanafunzi mmpatie morali kiongozi wenu; ni kiongozi mchapakazi na hawa ni wale ambao tunawaangalia kurudi tena hapa kwa sababu ni mchapa kazi.

(Applause)

Nataka niwaambie, na najua katika nyinyi wanafunzi yuko mmoja wenu ambaye atakuja kukaa hapa. Huenda akachaguliwa siku zijazo kuja kukaa hapa. Kwa hivyo, msione kwamba kuwa mheshimiwa ni kazi ngumu. Ni bidii yako ya kukaa na wananchi pamoja, kushirikiana na wazazi wako na kushirikiana na wananchi. Karibuni, nafikiri maaskari wale mnaowaona pale, Spika akiwaambia *Majority Leader* atoke nitabebwa juu juu katika Bunge hili na ni sheria na ni lazima wasikie sheria ya Spika anasema nini.

Hili ni Bunge la nidhamu na mkiwa na swali lolote mkitaka kuuliza mtaambiwa lolote mnalotaka kusikia, tuko na maafisaa wetu wachapa kazi watawaelezea. Asante, Bw. Spika, na Mwenyezi Mungu awabariki nyinyi wanafunzi na ndugu zetu wa SHOFCO. Karibuni sana.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. (Ms.) Meso: Thank you, Mr. Speaker, Sir. First of all, I would like to congratulate our Speaker, he has been the best Speaker for this year 2024. I would like to inform the students and the other group. I am called *mheshimiwa* Phillister Meso, Special Elect. I have advice for the students as a mother, as a matron of youth at St. Anthony Catholic Church Malindi for the last 20 years and dealing with youth is not easy but I manage because I also have youth in my house. So, the way I treat my children is also the way I am treating all youth. The advice I can give you students, first point; you must respect God. Without discipline you will go nowhere. You can get a very good grade but without discipline no one can employ you.

Another thing, you must work very hard. Hard work pays a lot. You must respect your teachers; you must respect your parents and you must respect your fellow students then you will make it. Education is the key to everything but without discipline, education is nothing. The way you are seeing us here, just as you have heard our Leader of Majority saying that he is giving us discipline, which is very true, you have just witnessed just now when one of us came in dressing in an awkward way. They forced him out of the Chamber, and he did it because he has discipline, and we must follow instructions from the Leader of the Majority.

I kindly beg you students to try your level best to have discipline and pray so hard so that God can hear your prayers. Prayers do miracles but you cannot keep on praying without doing your studies; do your studies and then keep on praying and all shall be well.

The other group, I congratulate you, welcome just the way our Leader of Majority has said, tomorrow His Excellency the Governor will be coming here, we would like *mheshimiwa* Paul, students to come here to see their Governor and the other group, we welcome you once more. It should not only be today, keep on coming to our County Assembly so that you can see how we are operating our business.

According to our Order Paper today, we really do not have any debating. Debate is the most important thing in the Assembly. Hon. Paul, make sure next week you go through the Order Paper and when you see there will be any Motion, then bring the students back so that they can know how to debate. Thank you so much, Hon. Speaker.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon.Hinzano...

(The Speaker spoke off record)

...we have some technical issues with our microphones including mine. If possible, you can use that one for the time being. Put on that one close to the Majority Whip. Just put the microphone on. Close please, yes use that one.

Hon. Hinzano: Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia hii nafasi. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge hili. Pokeeni salamu kutoka kwa Raisi wa Jamhuri ya Kenya Mheshimiwa William Ruto. Jana tulikuwa sote kwa kikao kule Ikulu na amewafurahikia sana na wito wake ni kwamba tuweze kushirikiana na viongozi tusianzishe siasa huu si wakati wa siasa, tufanye kazi kwa ajili ya wananchi wa Jamhuri ya Kenya.

(Applause)

Kwanza kabisa, nataka nichukue nafasi hii kupongeza washirika waliokuja na pia wanafunzi kwa kufika katika Bunge hili. Mimi wangu ni wasia tu kwa wanafunzi. Maisha

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ambayo mnayaona kwa familia zenu, hakuna mtu ambaye anaweza kuyabadilisha isipokuwa nyinyi mzingatie elimu. Hakuna jambo la miujiza wala maajabu litatokea kubadilisha familia zenu; ni nyinyi wenyewe ndio ambao mnaweza kubadilisha familia kupitia elimu. Nataka kuwaambia hivi; hakuna jambo rahisi na jinsi munavyong'ang'ana kwa masomo, Mwenyezi Mungu anawaona na atawashika mkono.

Mlikuwa na marafiki mlipokuwa katika shule za chekechea mkawaacha, mkaenda shule za upili mkawa na marafiki mkawaacha, sasa hivi mko shule ya upili mtawaacha hao marafiki ambao mko nao, mkienda *college* pia marafiki mtawaacha wale mtabahatika kuenda *university* pia marafiki mtawaacha lakini elimu ukiwa nayo huwezi kuiacha wala kushirikisha mtu mwengine katika maisha yako.

Nawambia hivi, kuna anasa nyingi ambazo zimejaa lakini ni za muda. Ile anasa ya kweli na uhakika ya kukusaidia kimaisha ni ya kuzingatia elimu. Mzingatie elimu mshirikiane na walimu na muwe makini katika maisha yenu. Mimi nataka niwahakikishie jambo moja, kwamba hatua ambayo mumefuata ya kufika Bunge hili ni jambo la muhimu sana. Ninaamini kabisa kitendo hiki mtakikumbuka katika maisha yenu kwa sababu baada ya hapa mtaenda kuwa na muongoza mpya wa kuwaongoza jinsi ambavyo mtakuwa mnasimama kimasomo. Nataka niwashukuru sana kwa kufika kwenu. Mimi kwa jina langu naitwa mheshimiwa Morris Hinzano, Wadi ya Kakuyuni. Nimechaguliwa kupitia chama cha UDA (*United Democratic Alliance*) peke yangu katika *Sub-County* ya Malindi kwa hivyo muwache kutishwa na watu; hakuna lisilowezekana. Mtu asikuwekee vizuizi kwamba hili jambo haliwezekani. Jambo lolote ambalo utaamua na ukiwa na nia utapata njia ya kufika. Kwa hivyo, muwe makini kwa maisha yenu na muwe na heshima kwa walimu na wazazi kwa sababu wazazi ndiyo humpa baraka. Asanteni sana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Yes, the Deputy Minority Whip, she should be summing up. I know everybody wants to speak but let her sum up for other business.

Hon. (Ms.) Radhia: Asante, Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii kama mama na mimi nikaweza kuwasalimia wanafunzi na kuwapongeza na pia shirika ambalo liko hapo juu.

Mimi nimesimama, mengi yamezungumzwa lakini nataka kuwaambia wanafunzi kuwa kina mama tunaweza na ndio hivi tumeweza. Kama Mheshimiwa wa Kakuyuni alivyosema, kila jambo lawezekana. Ni bidii na kuwa makini katika maisha yako. Sasa hivi mko *Secondary*, inaaminisha ukimaliza hapo ndo maisha yanaanza. Kwa hivyo, hapo ulipo ni uwe makini ujue waenda wapi. Maana hivi ni ujue bila elimu hakuna kitu; kwa hivyo mtu asikudanganye akisema kuna maisha baada ya kuwa mtu hakusoma, saa hii mtu atakuwa anakudanganya anakupoteza.

Zamani mtu alikuwa akifika *class eight* ukiambiwa nenda *form four*, ukifika *form four* wapata kazi lakini wacha niwaambie ukweli, saa hii kazi ya *form four* ni ya shilingi elfu kumi na tano ama elfu kumi na mbili. Kwa hivyo, shilingi 12,000 sasa hivi munavyojua nyinyi wenyewe hapo mukiwa sekondari shilingi 12,000 ni *pocket money* yenu, je utaweza wewe kuishi na shilingi 12,000 maisha ikiwa ni mke uzae na watoto wataka kushughulikiwa kwa shilingi 12,000 maisha yatazidi kuwa magumu na umaskini utaendelea.

Kwa hivyo, bila ya kusoma na kupita, kuna kusoma na kupita masomo. Bila kupita inaaminisha, bado umaskini kwetu utajaa. Kwa hivyo, mimi nawahimiza wanafunzi mfanye bidii sana katika mitihani yenu mwache mchezo. Hayo maisha ya kuitwa mwanafunzi yataisha; utaenda kuwa mama hapo ulipo kama sisi hapa tulipo. Mimi nimesimama kuwashukuru walimu wa hiyo shule ikaweza kuwaleta wanafunzi hapa. Hapa mmekuja kusoma, hamkuja kutembea. Mmetoka Magarini mkafika hapa, uende kujisifu leo umeenda Bunge, umeona nini Bungeni?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Lazima ukitoka hapa uwe umesoma moja, mbili, tatu. Kwa hivyo, wanafunzi *especially* hapa naona wanafunzi wa kike ya kwamba sisi akina mama tunaweza na wamama ndio kila kitu. Hata kwa dini yetu pia aliulizwa mtume wetu Mohammed, akaambiwa baina ya mama na baba nani zaidi akasema mama, akaulizwa tena akasema mama, akaulizwa tena akasema mama mara ya tatu ndio mara ya nne akasema baba.

Kwa hivyo, sisi tuna majukumu zaidi na zaidi kwa kizazi kijacho. Kwa hivyo, nyinyi pia mtakuwa kina mama na mtakuwa na watoto na mtajukumika. Langu zaidi ni kuwapongeza na kuwafanya muwe na bidii kweli kweli. Waliokuwa Waislamu hapo juu msidanganywe mkaambiwa Waislamu hawawi waheshimiwa, tayari mimi ni Muislamu nafuata sheria za dini na ni kipindi changu cha pili na tena nitarudi tena mwaka ujao Mungu akipenda.

(Applause)

Mimi ni mama niko na miaka hamsini (50) kuendelea lakini mpaka nimalize sabini (70) ndio nitoke kwa hii Bunge; sijui mmenielewa wanafunzi wangu? Kwa hivyo, mfanye bidii mjue Waislamu, Wakristo wote roho ni moja na wote tunaweza.

Wageni mlioko hapo juu, mashirika naona mmetuona vizuri hapa Bunge letu kama alivyosema *Majority* ni Bunge la sheria. Tuna utaratibu na ustaarabu na sisi wote hapa ni ndugu na ni marafiki. Mjue mkifika kule kazini, watu wanakuwa marafiki na mandugu. Mnaona pale na ndio urafiki unaendelea, kama sisi hapa sote tuko sawa hakuna ubaguzi wa rangi wala ubaguzi wa dini wala ubaguzi wa ukabila. Mimi wasia wangu kwenu, mkifika huko mwendako muwe na utaratibu kama wetu.

Kwa hayo mengi au machache nashukuru, Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia ningependa kukupongeza mheshimiwa wetu kwa kuvuka mshindi wa kwanza Kenya nzima kuwa Spika bora na vile vile mimi nasema leo tumeanza saumu yetu ya Ramadhan, tunaomba mambo yetu yawe mazuri *Inshallah* na nyinyi wenzetu pia mtuombee tufunge kwa salama, na tumalize kwa salama. *Asalam alekum.*

The Speaker (Hon. Mwambire): Asanteni sana waheshimiwa, kwa maneno ya busara mliowapatia wanafunzi wetu na wageni wetu. Wale pengine wamekosa kunukuu kwa sababu ya mazingira yaliyoko; waheshimiwa wamewatia imani na kama wamewatia imani, wamesema kwamba hakuna lisilowezekana kukiwa na imani. Imani ikiweko kila kitu kitakuwa sawa. Kwa hivyo, karibuni sana. Kama nilivyonukuu kwa lugha ya Kiingereza, karibuni sana nyote. Pia, changa moto ni kwenu, kama wamesema hakuna lisilowezekana, mtu asikutishe kama ilivyosemwa na Mwakilishi wa Wadi ya Kakuyuni. Mama amesema kwamba atakaa hapa mpaka zaidi ya miaka 70. Kwa hivyo, nyinyi vijana mchukue hiyo changamoto, msitishike na hilo, mjipange. Karibuni sana.

Kwa wale waheshimiwa wamenipatia pongezi, asanteni lakini tutaongea zaidi katika kipindi kijacho kile cha mchana. Ndio tutakuwa tukitoa habari maalumu kuhusu maswala hayo. Lakini kwa sababu kuna wageni, pengine hawatakuwa hapa. Asanteni sana kwa kongole zenu. Lakini yote yaliwezekana kwa ushirika wetu sote na kwa wale ambao tunawahudumia. Asanteni.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

PAPERS LAID

The Speaker (Hon. Mwambire): Is the Chairperson for Budget and Appropriations Committee in the House? I can see the Vice-Chairperson is around. Kindly, pass him the microphone.

REPORT OF THE BUDGET AND APPROPRIATIONS COMMITTEE ON THE COUNTY FISCAL STRATEGY PAPER (CFSP), 2024

Hon. Said: Asante sana, mheshimiwa Spika. Pia mimi kabla sijasoma *Order* yangu nataka pia nipongeze mheshimiwa Paul kwa kuweza kuleta wanafunzi hapa Bungeni. Kwa hivyo, mheshimiwa Paul, pia tunakuomba sana kwa sababu Gavana atakuwa hapa Bungeni uweze kuregesha wanafunzi hapa. Asante sana, wacha nisome Ripoti yangu, *order number five*.

Mr. Speaker, Sir, I beg to lay the following Report on the Table: -

Report of the Budget and Appropriations Committee on the County Fiscal Strategy Paper (CFSP), 2024. Thank you.

(Hon. Said laid the document on the Table)

The Speaker (Hon. Mwambire): Okay, you will forward it to the Clerk as required. The next one, please. The Chairperson of the Transport and Public Works Committee. Give him the microphone, please.

REPORT OF THE TRANSPORT AND PUBLIC WORKS COMMITTEE ON THE STATUS OF GROUNDED VEHICLES IN THE COUNTY

Hon. Mkadi: Thank you, Mr. Speaker, for this opportunity. I beg to lay the following Paper on the Table: -

Report of the Transport and Public Works Committee on the status of grounded vehicles in the County. Thank you.

(Hon. Mkadi laid the document on the Table)

The Speaker (Hon. Mwambire): Okay, you will share the Report with the Clerk as required. The next one is the Chairperson for the ICT and Research Committee, please give the microphone to the Chairperson, the one tabling. I can see hon. Faith is already upstanding. Yes!

Hon. (Ms.) Faith: Thank you, Mr. Speaker. First, I want to thank God for today for giving us good health. We are here at the Assembly, and I also want to welcome the visitors from the SHOFCO Organization and the students from Mjanaheri. I want to personally say, welcome to the County Assembly of Kilifi. My name is Faith Jane Kea, Special-Elect.

REPORT OF THE ICT AND RESEARCH COMMITTEE ON THE STATUS OF ICT CENTRES IN KILIFI COUNTY

Hon. (Ms.) Faith: I beg to lay the following Paper on the Table: -

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Report of the ICT and Research Committee on the Status of ICT Centres in Kilifi County.
Thank you, Mr. Speaker.

(Hon. (Ms.) Faith laid the document on the Table)

NOTICES OF MOTION

ADOPTION OF THE REPORT OF THE BUDGET AND APPROPRIATIONS COMMITTEE ON THE COUNTY FISCAL STRATEGY PAPER (CFSP), 2024

Hon. Said: Mr. Speaker, Sir, I beg to give Notice of the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the County Budget and Appropriations Committee on the County Fiscal Strategy Paper (CFSP), 2024 laid on the Table of this House on Tuesday, 12th March 2024.

Thank you.

ADOPTION OF THE REPORT OF THE TRANSPORT AND PUBLIC WORKS COMMITTEE ON THE STATUS OF GROUNDED VEHICLES IN THE COUNTY

Hon. Mkadi: Thank you, Mr. Speaker. I beg to give Notice of the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the Transport and Public Works Committee on the status of grounded vehicles in the County laid on the Table of this House on Tuesday, 12th March 2024. Thank you.

ADOPTION OF THE REPORT OF THE ICT AND RESEARCH COMMITTEE ON THE STATUS OF ICT CENTRES IN KILIFI COUNTY

Hon. (Ms.) Faith: Thank you, Mr. Speaker. I beg to give Notice of the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the ICT and Research Committee on the Status of ICT Centres in Kilifi County laid on the table of this House on Tuesday 12th March 2024.

Thank you, Mr. Speaker.

ADJOURNMENT

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, there being no other business to transact, the House stands adjourned until in the afternoon at 2:30 p.m. Thank you.

The House rose at 10:09 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*